# AMANI INAANZA NA SISI!

(mwongozo mdogo kwa vijana wajenzi wa amani)

WeWorld
Member of ChildFund Alliance

# Amani inaanza na sisi!

*Mwongozo mdogo kwa vijana wajenzi wa Amani.*

*Kijitabu hiki ni sehemu ya Mradi wa Kujenga Amani Pamoja (Building Peace Together) unaofadhiliwa kwa pamoja na Umoja wa Ulaya (European Union) na kutekelezwa na WeWorld katika nchi za Kenya, Tanzania, na Msumbiji. Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano na Tanzania Building Future Organization (TABUFO), 4H Tanzania, Stretchers Youth Organisation (SYO), na Conselho Nacional do Voluntariado (CNV). Kijitabu hiki kimetengenezwa mahsusi kwa ajili ya watoto, kwa lengo la kuwasaidia wawe watu wa Amani, wenye ujasiri na ushiriki katika maisha yao ya shule na ya jamii kwa ujumla. Kupitia hadithi, michezo, na tafakari, kinawahamasisha watoto kuchunguza maadili muhimu kama vile haki, demokrasia, amani, na heshima, na kuwasaidia kukuza ujuzi unaohitajika ili kuwa washiriki hai katika kujenga mazingira yanayowazunguka kuwa jumuishi, salama, na yenye Amani.*


Kamati Kuu ya Usimamizi ya WeWorld

Aneta Jelinkova (Mwakilishi wa Nchi Msumbiji); Annarita Spagnuolo (Mwakilishi wa Nchi Kenya); Camilla Capasso (Muhusika wa mawasiliano SEA); Dora da Nelete Arlindo (Mratibu wa Mradi Cabo Delgado); Dickson Okong'o (Mkurugenzi Mtendaji SYO); Elena Modolo (Mtaalamu wa masuala ya Elimu Duniani); Elvis Namajojo (Meneja wa Programu TABUFO); Francesco Corvatta (Msaidizi wa Mradi ESC); Fred Christopher Odera (Mratibu wa Mradi Kwale); Gaia Geoni (Mwanafunzi wa Mafunzo-Kituo cha Utafiti ); Ilaria Castelli (Afisa Msaidizi wa Utafiti); Ilaria Citerei (Meneja wa Eneo- Cabo Delgado); Job Mutombene (Afisa Msaidizi CNV); Joseph Desideri (Meneja wa Programu 4H Tanzania); Joseph Karinga (Afisa Mradi SYO); Julius James Katani ( Afisa Ufuatiliaji, Tathmini, Uwajibikaji na mafunzo); Mariana Cassimo ( Afisa wa eneo Cabo Delgado); Massimo Baraglia (Mwakilishi wa Nchi Tanzania); Martina Albini (Mratibu wa Kituo cha Utafiti); Miralda Sebastiao (Afisa Mradi Cabo Delgado); Mohamed Ally (Mkurugenzi Mtendaji TABUFO); Mwanahamis Saidi (Afisa Mradi 4H Tanzania); Rachele Ponzellini (Mratibu wa mawasiliano kwa ajili ya uelewa na mipango ya kimataifa); Rebecca Romagnoli (Afisa Mradi wa Kanda); Roberto Luciani (Msaidizi wa Mradi ESC); Rosa Tolla (Meneja wa Programu Mozambique); Sheila Sirali (Afisa Mawasiliano Kenya); Siria Pastorelli (Mwanafunzi wa Mafunzo-Kituo cha Utafiti); Tiziano Codazzi (Mtaalamu wa Chapa na Mawasiliano ya Muonekano ); Veronica Didas Kapinda (Mratibu wa Mradi Mtwara); Zacharia Buswelu Msabila (Mratibu wa Mradi Tanga); Zoe Fallon (Msaidizi wa Mradi ESC).

Kimeandikwa na Claudia Bellante

Maandishi ya awali na: Daniela Riva (Mratibu wa Mradi wa Kikanda)

Kimetafsiriwa na Stanslaus Nkalanga

Michoro na Ludovica Sodano

Ubunifu wa muonekano na Marco Binelli

Kimeandaliwa na WeWorld
www.weworld.it/en



*Kinasambazwa bure: Maandishi ya chapisho hili yanaweza kunukuliwa tu kwa kutaja chanzo.*



*Chapisho hili limekamilika Oktoba 2025.*

KUJENGA AMANI program building peace together — CNV moçambique — Stretchers Youth Organization — TABUFO — 4HTANZANIA — Co-funded by the European Union

*Chapisho hili limetolewa kwa msaada wa kifedha kutoka Umoja wa Ulaya. Maudhui yake ni jukumu la WeWorld pekee na hayaakisi maoni ya Umoja wa Ulaya.*




KUJENGA AMANI program
building peace together

WeWorld
Member of ChildFund Alliance

Hamjambo wote! Tumeshawahi kukutana?

Kama bado, nafurahi kukutana nanyi!

Kwa kuanza, naomba tujitambulishe kwa kifupi sisi wenyewe, sawa?





Mimi naitwa **Hamisi**, nina umri wa miaka 9, ninatokea nchini Kenya, nina dada wawili ambao ni.... tuseme safii. Ninapenda kukimbia, kucheza bao, na kula ugali uliopikwa na bibi yangu.



Mimi naitwa **Amina**, nina umri wa miaka 12, Ninatokea nchini Tanzania. Ninapenda kutumia muda mwingi nikiwa na kaka yangu mkubwa na kucheza rede na marafiki zangu.



Mimi naitwa **Mariana**, nina umri wa miaka 14, Ninatokea nchini Msumbiji. Ninapenda kutazama nyota usiku na kuruka kamba huku nikicheza na wenzangu wa shule.

Amina: Ingawa tunatoka sehemu tofauti na tuna umri na simulizi tofauti, bado tuna mambo mengi yanayofanana.



Hamisi: Tunaamini katika mazungumzo na tunachukia vita kwa mioyo yetu yote!

Mariana: Kwa mfano, tunapenda kupaza sauti zetu pale tunapoona mambo hayapo sawa, tunaomba watu wazima waheshimu haki zetu na kututendea vyema, tunataka kushiriki kikamilifu na kubadilisha dunia kuwa mahali salama.




Je, mambo haya yanasikika kama ya watu wazima tu? Hapana, sio sahihi! Na kama ungependa kutumia muda wako pamoja na sisi, tutakuelezea ni kwa nini.

Shukrani kwa kijitabu hiki kidogo chenye rangi nzuri, kilichosheheni michezo na maswali, kitakusaidia kukua hadi kuwa mwanachama jasiri, hai, na mpenda amani katika shule na jamii yako.




Tutakusaidia kujifunza kuhusu wajibu wako na haki zako, na tutakushirikisha baadhi ya mbinu za kushughulikia migogoro kwa amani.



# Je, ni nini maana ya kuwa Raia Mshiriki/Hai?



Kuwa **raia mwamirifu (mshiriki)** maana yake ni kuwa mtu anayewajali wengine na anayechangia kuboresha jamii.





Lakini ili kufanya hivyo, kufuata sheria tu pekeake haitoshi! Lazima uhakikishe kwamba kila mtu anahisi yupo salama, anaheshimiwa, na anajimuishwa.








Mariana: Kuwa raia mshiriki pia inamaanisha kujua **haki zako, majukumu yako na wajibu wako.**



## Lakini haki ni nini?

### Haki za binadamu

ni mambo ambayo kila mtu anahitaji ili kuishi kwa usalama, kwa furaha na kiafya.

Ni za kila mtu, haijalishi unatoka wapi, unazungumza lugha gani, dini yako, kabila lako au tamaduni yako, kama wewe ni msichana au mvulana, au una umri gani.







Lakini maadamu sisi ni watoto na hatujafikisha umri wa miaka 18, tuna haki maalum!

## Haki za watoto

zinasema kwamba tunapaswa kusikilizwa, kwenda shule na kujifunza, kuishi kwa amani, kupata msaada tunapokuwa wagonjwa, kuwa na muda wa kucheza na kupumzika, na kutendewa kwa wema na heshima.





Haki zote hizi zipo kwenye Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto, ni hati muhimu iliyoandaliwa na kuandikwa na serikali zote za nchi zinazotaka kulinda haki zetu.




**MUHIMU!** Haki zote zimeunganika, kwa usawa zote ni muhimu na haziwezi kuondolewa.



**TAZAMA!** Ukiruka hadi katikati ya kitabu, utakutana na mabango mawili ambayo unaweza kuyachana na kuyatoa. Yatundike popote unapopenda.

Muhimu ni kwamba watu wazima pia wataweza kuyaona, na hivyo watakosa visingizio zaidi vya kutoheshimu haki zetu!

"Samahani, lakini kwa kweli sijui ni nini maana ya serikali..."





**Serikali** ni kikundi cha watu ambao kazi yao ni kuongoza nchi.

Hufanya maamuzi juu ya sheria muhimu, huaandaa na kutoa huduma (kama vile shule na hospitali) na inachukua jukumu la kutatua matatizo yanayoathiri wananchi wote.

Serikali nzuri husikiliza, hufanya maamuzi na kujaribu kuhakikisha kwamba watu wanaishi pamoja kwa amani.




"Na vipi kuhusu Umoja wa Mataifa?"
Umoja wa Mataifa ni shirika linazozileta kwa pamoja nchi nyingi kutoka sehemu mbalimbali za dunia na huzisaidia kudumisha amani kwa kuhamasisha serikali kushirikiana katika kutatua matatizo yanayoikumba dunia.
Je, Kenya, Msumbiji, na Tanzania pia ni sehemu yake?
Ndio
KENYA
TANZANIA
MOZAMBIQUE
Safi sana!


Kwa hiyo, tunapofikisha umri wa **miaka 18**, je, haki zetu za watoto zinatoweka?



Hapana! Haki hizo hazipotei; bali unaongezewa haki nyingine mpya kwa sababu unakuwa mtu mzima. Kwa mfano, unaweza kupiga kura kwenye uchaguzi na kufanya maamuzi yako mwenyewe.

Hizi ni haki nzuri na muhimu, lakini pia zinahitaji uwajibikaji zaidi: maamuzi yako yanakuwa ya maana sana, na ukikosea, unapaswa kujifunza kukabiliana na matokeo.





# Majukumu na wajibu

**Shiriki:** Watashiriki kwenye; Vilabu vya shule, Miradi ya kijamii, Vikundi vya vijana.





**Paza sauti yako:** Toa maoni yako, Uliza maswali.

**Simama** kidete kutetea yaliyo ya haki na kuwasaidia wale wanaotendewa kinyume cha haki.






**Kuwa na taarifa** kuhusu kile kinachotokea katika jamii yao.



**Wasaidie** wale walio kwenye matatizo.



**Jenga amani na urafiki**
Tatua migogoro kwa njia ya amani na saidia kila mtu ajisikie kuwa amejumuishwa, ili jamii ibaki kuwa imara na yenye amani.

**Kufanya mambo haya kunatupa nguvu, nguvu iliyo chanya, nguvu ya kufanya mambo kuwa bora!**



Nini maana ya “nguvu”?



Ni uwezo wa kufanya maamuzi na kuwezesha mambo yatokee, hasa mambo mazuri!

Lakini nguvu si ni kitu ambacho watu wazima tu ndio wanacho?

Si hivyo tu. Hata kama inonekana ya kuwa wao ndio wanaofanya maamuzi muhimu, tuna haki ya kusikilizwa, hasa jambo linapokuwa linahusu maisha yetu. Maoni yetu ni muhimu!



Kutoa maoni yako haimaanishi kupiga kelele, bali ni kushirikisha mawazo yako kwa uwazi, kuwasikiliza wengine na kutafuta njia za amani na utulivu pale mnapokosa kukubaliana wakati wa majadiliano.




**Lakini maneno peke yake hayatoshi! Vitendo vinahitajika pia!**







# Simulizi fupi za watoto werevu zenye mafunzo makubwa



## TANZANIA

Mimi naitwa Neema, nina umri wa miaka 14, na mimi natokea Tanzania kama Amina. Mojawapo ya mambo ambayo yananitia wasiwasi zaidi ni kudanganywa na mtu mzima, kulazimishwa kufanya kazi, au kuuzwa ili wengine waweze kupata pesa. Siku moja, nilipata ujasiri na nikaenda kuzungumza na mwalimu wangu, ambaye alinitia moyo na kunishauri nizungumze na jamii yangu yote kuhusu jambo hilo. Watu wazima walinisikiliza, marafiki zangu wengi walikuwa na hofu hiyo hiyo, na ninashukuru kutokana na mkutano ule, sasa tuna mabango kadhaa yaliyobandikwa shuleni ambayo yanatusaidia kutambua viashiria hatarishi na kuelezea jinsi gani na kwa nani tunaweza kuripoti. Kwa kuongezea, nilianzisha kikundi cha wasichana ambapo tunaweza kuongea kwa uhuru kuhusu mambo hatarishi na matukio ambayo yametupata sisi wenyewe au wengine, na viongozi wa serikali za mitaa wanatuunga mkono.



## TANZANIA

Jina langu ni Abdallah, nina umri wa miaka 13, wasiwasi wangu mkubwa ni hofu inayotukumba pale tunapokabiliana na polisi, ambao mara nyingi sio wema na wenye heshima kwetu. Nilizungumza kuhusu hili na jamii, na kwa sasa mazungumzo yameanzishwa kati ya wananchi na polisi, na hapa kijijini sasa hivi tunajihisi salama zaidi na hofu imepungua.







## MSUMBIJI

Mimi naitwa Ernesto, nina umri wa miaka 13, na siku moja niliamua kuandika ombi/ lalamiko (hati au nakala ya kuomba kitu kibadilishwe, na watu wengi huweka sahihi) kwa sababu nilikuwa nimechoshwa na hatari na hofu ya kugongwa na gari kila mara ninapokuwa ninaenda shuleni. Wanafunzi wenzangu walikubaliana nami na pia wakasaini ombi hilo. Kwanza tuliliwasilisha kwa kamati ya shule, baadaye tukalipeleka kwa viongozi wa kijiji. Matokeo yake ni kwamba sasa hivi tuna watu wazima zaidi wanaotusaidia njiani tunapoenda shule, na kituo cha basi kimehamishwa kwenda mahali salama zaidi kwa ajili yetu wanafunzi.



## MSUMBIJI

Jina langu ni Celeste, nina umri wa miaka 15, na nililazimika kuondoka nyumbani kwetu kaskazini mwa Msumbiji kwa sababu ya migogoro yenye vurugu. Mahali ninapoishi sasa, nilijiunga na "Klabu ya Amani" shuleni na ninatumia maigizo na mashairi kusimulia hadithi yangu. Hii inawatia moyo watoto wengine wengi ambao, kama mimi, walilazimika kuzikimbia familia na makazi yao. Sanaa imetusaidia kutuponya, lakini pia kuelewana na kusaidiana.









## KENIA

Mimi naitwa Rahmina, na nililelewa na kukulia katika mji wa bandari ya Kisumu ulioko karibu na Ziwa Viktoria, na tangu nilipokuwa na umri wa miaka mitano nimekuwa nikijhusisha na utunzaji wa mazingira katika eneo langu. Nilipokuwa mtoto, nilikuwa napanda miti na mama yangu na kuifuatilia ikikua na kuwa mikubwa na imara. Mwaka 2017, nilipokuwa na umri wa miaka 15, magugu maji mazito yaliyoitwa "water hyacinths" yalianza kusambaa ziwani, ndipo nikaanzisha kampeni ya "Acha Ziwa Victoria Lipumue Tena" (Let Lake Victoria Breathe Again) ili kuongeza ufahamu wa wanafunzi kuhusu athari za mabadiliko ya hali ya hewa (tabianchi) na haja ya kurejesha mfumo wa ikolojia wa ziwa.Kampeni hii ilipelekea kuanzishwa kwa Kinara wa Mazingira Kisumu, kundi la vijana wapenda mazingira, pamoja na kuanzishwa kwa Rahmina Paulette Eco-Products, biashara ndogo inayotengeneza bidhaa rafiki kwa mazingira kutokana na magugu maji na kutoa ajira kwa wanajamii.

## QUÉNIA

Mimi ninaitwa Sarah, nasoma Shule ya Msingi ya Matuga iliyopo katika Kaunti ya Kwale. Baba yangu alipofariki, nilijihisi mpweke na kuvunjika moyo. Natoa shukrani zangu kwa Klabu ya Amani na mwalimu wangu, nilipata faraja katika dansi na sanaa. Kwa sasa mimi ni kiongozi wa Klabu ya Amani, na tunajitahidi kuhamasisha na kudumisha amani, kila mara kwa kutumia njia za kibunifu katika kufanya uponyaji na maridhiano.






Simulizi hizi ni nzuri kama nini! Sasa ninaelewa mlichomaanisha! Na wewe unayesoma hapa, je, umeelewa pia?



Basi hebu tucheze mchezo! Kwa kweli, michezo miwili!



## Huu hapa ni wa kwanza:

- Chora mchoro unaoonyesha jambo fulani zuri ambalo umelifanya au ungependa kulifanya, na uandike pembeni yake jambo hilo linahusu nini.

- Bandika mchoro wako darasani au uwashirikishe na wana Klabu wenzako wa Amani!

- Ungana na rafiki yako na mje na mawazo mapya ya mambo ambayo mnaweza kuyafanya.

- Andika au chora mawazo yenu mapya kisha yashirikishe kwa wanadarasa kwa kuyabandika kwenye ukuta shuleni mahali ambapo watu wengi hupita.

Huo utakuwa ukuta mkuu wa raia hai na utawahamasisha wale wote watakaouona!


## Huu hapa ni mchezo wa pili:

- Katikati ya kijitabu hiki, kuna bango la haki. Chagua haki unayopenda zaidi au inayoonekana kuwa na umuhimu sana kwako. Kisha, tunga hadithi kuhusu mtoto ambaye haki yake haiheshimiwi na uelezee kile wanachoweza kufanya ili wazungumze na kujilinda.

- Ili kuhamasisha zaidi, unaweza kahadithia simulizi kutoka kwenye jamii yako au kutunga simulizi yako mwenyewe kwa kutumia fikra zako!

- Wakati wewe na wanadarasa wenzako mmemaliza kuandika simulizi zenu, mnaweza kuzikusanya katika kitabu, na kuandaa kitabu cha kwanza cha

**watoto wazuri na haki zinazoheshimiwa!**



# Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto Umeainisha Haki 42 za Watoto. Hizi ni baadhi ya Haki Hizo. Bandika mabango haya darasani kwako, nyumbani, kwenye Klabu ya Amani... au mahali popote unapofikiria panafaa, ili kila mtu aweze kuyaona!



**Ibara ya 1. Maana ya Mtoto**
Mtoto ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka kumi na nane (18).

**Ibara ya 2. Kutokubaguliwa**
Watoto wote wana haki sawa bila kubaguliwa, haijalishi mtoto anatokea wapi, anazungumza lugha gani, ana dini gani, anaonekana vipi, ni mvulana au msichana, ana ulemavu au hana, ni maskini au tajiri, au wazazi wake ni wa kina nani. Mtoto yoyote hapaswi kutendewa vibaya kwa sababu yoyote ile.







**Ibara ya 6. Kuishi na Kuendelezwa**
Kila mtoto ana haki ya kuishi na kuendelezwa. Serikali lazima zihakikishe kuwa watoto wanaishi na kukuzwa katika njia bora. Watoto wanapaswa kupata lishe bora, chanjo za magojwa, mavazi, makazi salama, na elimu ili waweze kuishi na kukua vizuri.

**Ibara ya 8. Utambulisho**
Kila mtoto ana haki ya utambulisho wake mwenyewe - rekodi rasmi ya kuwa yeye ni nani ambayo inajumuisha jina lake,




utaifa na mahusiano ya familia. Hakuna mtu anayepaswa kuchukua utambulisho wake, lakini ikiwa hii itatokea, serikali lazima isaidie kurejesha utambulisho wake kwa haraka.



**Ibara ya 3 na 18. Maslahi Bora ya Mtoto na Wajibu wa Wazazi**
Watu wazima wanapofanya maamuzi, wanapaswa kufikiria ni kwa namna gani maamuzi yao yatawaathiri watoto. Watu wote wapaswa kufanya yale yaliyo bora kwa watoto. Wazazi ndio walio na jukumu kuu la kumlea mtoto. Ikiwa mtoto hana wazazi, mtu mzima mwingine atakuwa na jukumu hili na huwa wanaitwa "Walezi au Mlezi". Wazazi na walezi wanapaswa kila wakati kufikiria kile kilicho bora kwa mtoto. Serikali nazo zinapaswa kuwasaidia katika kazi hii. Ikiwa mtoto ana wazazi wote wawili, wote wawili wanapaswa kuwa na jukumu la kumlea mtoto.

**Ibara ya 12. Kuheshimu Maoni ya Watoto**



Watoto wana haki ya kutoa maoni yao kwa uhuru juu ya mambo ambayo yanawahusu. Hivyo, watu wazima wanapaswa kuwasikiliza na kuyafanyia kazi maoni hayo.

**Ibara ya 19, 32, 33, 34, 35, na 36. Kulindwa dhidi ya Ukatili, Kazi Hatarishi na Dawa za Kulevya, Unyanyasaji wa Kingono, Usafirishaji haramu wa Binadamu na Unyonyaji.**




Serikali zinapaswa kuwalinda watoto dhidi ya ukatili, unyanyasaji na kutelekezwa. Watoto wana haki ya kulindwa dhidi ya kazi ambazo ni hatarishi na zinazoharibu afya, elimu au ukuaji wao. Kama mtoto anafanya kazi, anapaswa kuwa salama na alipwe kwa haki. Serikali inapaswa kuwalinda watoto dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya na unyanyasaji wa kingono. Pia, serikali inatakiwa kuhakikisha watoto wanalindwa dhidi ya utekaji, kuuzwa, au usafirishaji haramu kwenda nchi au sehemu nyingine kwa ajili ya kufanyiwa mambo ya kinyonyaji.



## Ibara ya 17. Upatikanaji wa Taarifa

Watoto wana haki ya kupata taarifa kutoka kwenye mitandao, redio, runinga, magazeti, vitabu na vyanzo vingine. Watu wazima wanapaswa kuhakikisha kuwa taarifa wanazopata watoto hazina madhara hatarishi. Serikali inapaswa kuhamasisha vyombo vya habari kutoa taarifa kwa kupitia njia mbalimbali, na kwa lugha rahisi ambayo watoto wote wanaweza kuelewa.

## Ibara ya 23. Watoto Wenye Ulemavu



Kila mtoto mwenye ulemavu ana haki ya kuishi maisha mazuri na kushiriki kikamilifu katika jamii. Serikali zinapaswa kuondoa vikwazo au vizuizi vyote vinavyowazuia watoto wenye ulemavu kujitegemea na kushiriki katika shughuli za kijamii kama watoto wengine.



## Ibara ya 28. Upatikanaji wa elimu

Kila mtoto ana haki ya kupata elimu. Elimu ya msingi inapaswa kutolewa bure. Elimu ya sekondari na ya juu inapaswa kupatikana kwa kila mtoto kwa urahisi.Watoto wanapaswa kuhamasishwa kwenda shule hadi kiwango cha juu wanachoweza kufikia. Adhabu shuleni inapaswa kuheshimu haki za mtoto, na sio kumfanyia ukatili.

## Ibara ya 39. Kupona na kujumuishwa



Watoto wana haki ya kupata msaada ikiwa wameumizwa, wametelekezwa, wameteswa au wameathiriwa na vita, ili waweze kurejesha afya na utu wao.

## Ibara ya 22. Watoto Wakimbizi



Watoto wanaokimbia kutoka nchi yao kwenda nchi nyingine kwa sababu mbalimbali kama vile vita, wanapaswa kusaidiwa na kulindwa, na kupata haki zote sawa kama watoto waliozaliwa katika nchi hiyo.



## Ibara ya 24-27. Afya, Maji, Chakula, Mavazi na Mazingira Salama

Kila mtoto ana haki ya kupata huduma bora za afya, maji safi ya kunywa, chakula chenye lishe na mavazi ya kutosha. Kila mtoto pia ana haki ya kuishi katika nyumba yenye mazingira safi na salama. Serikali inapaswa kusaidia familia na watoto ambao hawana uwezo wa kupata mahitaji haya muhimu.

## Ibara ya 31. Kupumzika, Kucheza, Utamaduni na Sanaa



Kila mtoto ana haki ya kupumzika, kustarehe, kucheza na kushiriki katika shughuli za kitamaduni na kiubunifu.



## Ibara ya 38. Ulinzi Wakati wa Vita

Watoto wana haki ya kulindwa wakati wa vita. Mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 15 haruhusiwi kujiunga na jeshi au kushiriki vitani.

Lakini je, kutaka kuwa raia hai peke yake inatosha?

Sivyo kabisa. Kuna mambo mawili muhimu sana ambayo bila hayo itakuwa vigumu, kama sio haiwezekani, ili kufanya sauti zetu zisikilizwe na kugeuza mawazo yetu kuwa vitendo.



Na ni yapi hayo?



Ni demokrasia ya kweli na uchaguzi wa haki.



# Demokrasia ni nini?

**Demokrasia** ni njia ya kuendesha nchi au jamii ambayo watu wana nguvu ya kufanya maamuzi na kushiriki katika chaguzi ambazo huathiri maisha yao.

Katika demokrasia, kila mtu ana haki na uhuru sawa.

Demokrasia ni muhimu kwa sababu inasaidia watu kuishi kwa kuheshimiana, kujifunza na kukua, na kuishi kwa amani.

Demokrasia inamaanisha kufanya kazi kwa pamoja ili kufanya shule na jamii kuwa sehemu bora na yenye furaha kwa kila mtu.


Lakini je, pia kuna demokrasia kwa sisi watoto?



Bila shaka! Unaweza kutekeleza demokrasia kila siku kwa kujiunga na vilabu vya shule, kubadilishana mawazo wakati wa mikutano, kusikiliza wengine, kuchangia katika maamuzi ya kikundi, au kuwa sehemu ya baraza la wanafunzi.



Unajua, kwangu mimi demokrasia ni kama mti. **Mizizi** yake ni **maadili** yanayotokana nayo, **shina** lake ni **taasisi** zinazoiimarisha, na **matunda** yake ni mambo mazuri ambayo huleta kwa kila mtu katika jamii!



Je, ungependa kuchora na kupaka rangi mti wako sasa na kuandika ni maadili gani yanayoopaswa kuzingatiwa, ni taasisi zipi zinapaswa kuyashikilia, na matunda matamu zaidi ni yapi yanayopaswa kuvunwa? Ukimaliza, washirikishe marafiki zako na tengenezeni ukuta wa miti ya kidemokrasia!



**Hivyo, kumbuka:**
**Wakati tunatunza mizizi (maadili), shina (taasisi) inakua imara, na matawi (matokeo) husaidia kila mtu katika jamii!**



# Kwa nini uchaguzi wa haki ni muhimu?

Katika nchi ya kidemokrasia, watu huwachagua viongozi wao kwa kuwapigia kura na viongozi hao hutarajiwa kuwasikiliza watu na kufanya kile kilicho bora kwa kila mmoja.

**Uchaguzi** ni njia tunayotumia kuwachagua viongozi wanaotuwakilisha na ambao tunadhani wanaweza kufanya kazi iliyo bora kwetu, kama vile darasani kwenu mnavyopiga kura kumchagua mwakilishi wa darasa au wewe na marafiki zako mnavyomchagua nahodha wa timu mnapotaka kucheza mchezo.

## Tunapopiga kura, tunatumia sauti zetu.

Uchaguzi wa haki unahakikisha kwamba viongozi wanachaguliwa na kila mtu, na si kikundi kidogo tu, na uchaguzi ukiwa wa haki, watu huwa na uwezekano mkubwa wa kuheshimu matokeo na kushirikiana kwa ajili ya manufaa ya jamii nzima.



# Je, uchaguzi hufanyaje kazi katika demokrasia?

Ni rahisi!

1) Watu wanaweza kuwa wagombea



Kama wakitimiza umri unaohitajika na wanaamini kuwa wana uzoefu unaofaa, watu wanaweza kuamua kujitokeza na kuwa wagombea. Ili kupata kura, wanahitaji kuwashirikisha wapiga kura mpango wao wa kazi, kueleza mawazo yao na yale watakayofanya wakishinda.

2) Kampeni za uchaguzi



Wagombea hujielezea ni vitu gani watafanya ikiwa watachaguliwa. Hutoa hotuba mbele ya umma, hutembelea vijiji na jamii, hushiriki katika mijadala, ambapo wagombea hujadili na kulinganisha mawazo na maoni yao juu ya mada fulani, husambaza vipeperushi, na hubandika mabango. Haya yote huwasaidia wapiga kura kulinganisha mawazo na kuchagua mgombea.

3) Watu kupiga kura



Siku ya uchaguzi, watu huenda mahali panapoitwa kituo cha kupigia kura. Kila mpiga kura huchagua mgombea anayemfikiria kuwa ni bora zaidi. Katika demokrasia, kila kura ni sawa, bila kujali wewe ni nani.

4) Kuhesabu kura




Baada ya kila mtu kupiga kura, kura hizo huhesabiwa kwa umakini ili kubaini ni mgombea yupi amepata kura nyingi zaidi.

5) Mshindi anakuwa kiongozi






Mgombea aliyepata kura nyingi atatangazwa kuwa mshindi na anakuwa kiongozi kwa kipindi fulani kilichowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

# Viongozi wanapaswa kufanya nini katika demokrasia?

Katika demokrasia, kiongozi bora ni mtu anayesaidia kila mtu kufanya kazi pamoja na kuishi kwa amani.

**Uongozi bora** unapaswa kuambatana na **uwajibikaji** kila wakati.



**Uongozi** = Ni uwezo wa kuongoza na kuhamasisha kundi la watu kufikia lengo la pamoja, kwa kuwasikiliza, kuelewa hisia za wengine, na kuweza kufanya maamuzi yenye ufanisi.

**Uwajibikaji** = uwezo na wajibu wa kutoa majibu kuhusu matendo ya mtu, mwenendo wake, na matokeo yanayotokana nayo.

# Ni kwa namna gani unaweza kuwa kiongozi bora kijana na unatakiwa kufanya nini?

**Hata kama wewe si mtu mzima, bado unaweza kuwa kiongozi katika shule au jamii yako!**

**Ili kuwa kiongozi bora, ni muhimu:**

Kusikiliza kwa makini mawazo, masuala na maoni ya wengine.



Kuwa wa haki na mkweli kwa kila mtu, hata pale inapokua vigumu au hakuna yeyote anayekutazama.



Fanya maamuzi baada ya tafakari ya kina inayozingatia mahitaji ya kila mtu.



Kubali mrejesho na ujaribu kuboresha mambo unapokosea.



**Paza sauti pale jambo fulani linapotendwa isivyo haki, wakati marafiki zako wanapoumizwa, au wakati mtu anapotengwa na wengine.**



Wasaidie wengine kutatua matatizo kwa amani na uwe na heshima kwa wote.



Shirikisha mawazo mapya ili kuboresha maisha ya shule au shughuli za klabu.



Kuwa mwajibikaji: chukua jukumu kwa kile unachofanya.



Kuwa na taarifa ya kile kinachoendelea katika jamii yako na pia wasisitize viongozi kuwajibika kwa matendo yao.



Kuongoza kwa kutumikia; sikuzote kumbuka: “Mimi nipo hapa kuwatumikia, na si kuwatawala”. Kazi ya kiongozi ni kusikiliza, kutatua matatizo, na kuboresha maisha ya kila mtu, si kuamrisha watu au kufikiri wao ni muhimu zaidi kuliko wengine.




Viongozi bora huheshimu sheria na kamwe hawatumii mamlaka kwa manufaa ya marafiki au familia zao. Kiongozi akiwa na upendeleo kwa marafiki au familia tu, hii inaitwa ufisadi au mgongano wa maslahi.



Na sasa, hebu tuigize kufanya uchaguzi... na kufanya mabadiliko kama viongozi wa kweli! Je, mko tayari?




Ni rahisi na inafurahisha, lakini unapaswa kufanya kwa juhudi!



## HATUA:

Kwanza, **wagawanye katika vikundi vidogo na uchore ramani ya eneo lenu.** Kisha weka alama kwenye maeneo muhimu kama vile shule, nyumba zenu, soko, hospitali, kituo cha polisi, kanisa, msikiti... kuwa mbunifu! Tumia lebo zilizopo kwenye ukurasa unaofuata na fikiria nyingine mpya zinazowakilisha jirani yenu.

Sasa **angalia ramani yako kwa makini na ujiulize: ni nini tunaweza kuboresha**?

**Fikiria si majengo tu bali watu pia**. Je, kuna yeyote anayehisi ametengwa? Labda kwa sababu wana tatizo la kutembea...

Je, kila mtu anahisi kukaribishwa? Je, wana nafasi ya kucheza, kujifunza na kufanya kazi?

**Chagua tatizo moja au mawili ambayo unaona ya kuwa ni muhimu na myatafakari na kuzungumza kwa pamoja.** Ni hatua gani ndogo zichukuliwe ili kuboresha hali iliyopo? Je, kuna watu wazima ambao wanaweza kusaidia? Na kwa namna gani?

Halafu, **chagueni kiongozi wa kikundi chenu kwa njia ya kidemokrasia**! Mmeshakamilisha? Safi sana! Mtu huyu atakuwa mwakilishi wa kundi lenu katika uchaguzi.

Sasa, **msaidieni kutengeneza bango la uchaguzi**. Bango hilo linapaswa kuwa na picha yake, kaulimbiu ya kuvutia, na ujumbe wa kampeni ambao una mawazo makuu ya mpango wake wa uongozi.

**Onyesha bango hilo darasani huku kiongozi akitoa hotuba yake ya kampeni.**



Baada ya makundi yote kuwasilisha, tafakarini kwa pamoja: Je, kila mtu alikuwa na nafasi ya kuzungumza? Ni nini kilichofanya kazi ya timu au pamoja iwe rahisi au ngumu? Ni hatua gani zilizotumiwa kufanya uchaguzi uwe wa haki? Tumejifunza nini kuhusu uongozi na kazi ya pamoja? Sasa kwa kuwa tumeelewa maana ya kuwa raia hai, tunahitaji pia kujua kwamba kadiri tunavyoshirikiana kwa karibu, iwe nyumbani, shuleni, au katika jamii, ndivyo tunavyohitaji kujifunza namna ya kushughulikia tofauti za mawazo (migogoro), kwa sababu watu hawafikiri kwa njia ile ile. Na hilo ndilo jambo la kusisimua zaidi.




Kuwa na uelewa wa namna ya kusuluhisha migogoro kwa njia ya amani ndiyo ufunguo!




# Kujua jinsi ya kutatua migogoro kwa amani ni muhimu!



# Amani ni nini?

**Amani** ni zaidi ya "kutokuwa na mapigano" au kukosekana kwa vita. Amani humaanisha kwamba kila mtu anaheshimiwa, anajihisi yupo salama, na anaweza kuishi maisha yenye furaha na afya njema. Amani ni pale ambapo watu wana chakula cha kutosha, wanaweza kwenda shuleni, wana marafiki, na wanatendewa kwa wema.




**Amani yaweza na yapasa kuwa kila mahali.**

# Vipepeo vya Amani


## Hebu tucheze mchezo mwingine:

Funga macho yako na ufikirie amani inamaanisha nini kwako. Sasa andika neno la kwanza linalokuja akilini mwako kwenye kipepeo cha amani kilicho karibu yako. Kipige rangi, kinyenyue, na ukizungushe ili neno lako la amani liweze kupepea na kuwafikia watu wengine.



# Ujumbe wa Kanga

Kama hupendi kutumia kipepeo na huwa unapendelea kutumia Khanga ya kujifunga au hata kuihangika ukutani, hii hapa ni Khanga yenye rangi na unaweza ukaiandika maana ya amani kwako.




# Picha na maneno ya kukata na kubandika

Kata picha tatu unazoziona pembeni kisha uzibandike kwenye karatasi ili kutengeneza kola ndogo. Baada ya hapo, andika sentensi moja inayoelezea kwa nini kazi yako inawakilisha amani.




PEACE
PAZ
PEACE
AMANI











DIRA HOSPITAL













SCHOOL


Book














7
8
6
4
5
3
2
1



# Mgogoro ni nini na kwa nini hutokea?

**Mgogoro** hutokea pale watu wanapotofautiana au wanapotaka vitu tofauti. Unaweza kutokea ndani ya familia, kati ya marafiki, shuleni, kati ya jamii, na hata kati ya nchi.



**Kutokuelewana** kati ya watu ni sehemu ya maisha yetu ya kila siku lakini kwa kujifunza njia za amani za kutatua tofauti hizo, tunaweza kupata matokeo mazuri na kujifunza kuelewa mitazamo mbalimbali.



# Sababu za migogoro



## Tofauti za mahitaji

Pale tunapotaka au tunapohitaji kitu kilekile kwa wakati mmoja.



## Tofauti za maadili

Huweza kutokea pale tunapotofautiana kuhusu mambo tunayoyaona kuwa muhimu.

Mfano: mtoto mmoja anafikiri kuwa "kujisomea ndio jambo la muhimu zaidi", wakati mwingine anafikiri kuwa "kucheza michezo ndio jambo la muhimu zaidi".




## Tofauti za maoni

Hii Hutokea pale tunapoona mambo kwa njia tofauti.



**Mahusiano** Hii hutokea pale tunapopata hisia kali kama vile hasira au wivu katika mahusiano yetu na wengine.




**Miundo au mifumo ya haki na usawa** Hii hutokea pale panapokuwa na ukosefu wa haki na usawa kwa kila mtu.

# Migogoro na nguvu

Migogoro huwa migumu zaidi wakati nguvu zinapoanza kutumika, yaani, wakati mtu au kikundi kimoja kinapokuwa na nafasi zaidi, rasilimali zaidi, au sauti yenye nguvu zaidi kuliko wengine.

Kuna aina tofauti za nguvu:



**Nguvu ya Kiuchumi:** pale mtu anapokuwa na pesa au mali nyingi kuliko watu wengine.

**Nguvu ya kisiasa:** wakati wale wanaotunga sheria wanapokuwa hawasikilizi maoni ya kila mtu.



**Nguvu ya Kijamii:** mtu anapojaribu kuwalazimisha wengine waishi kulingana na desturi au mapokeo yake.






**Nguvu ya kitaaluma au akili:** wakati mtu anapokuwa na ujuzi wa mambo muhimu lakini hayashirikishi kwa wengine.



**Nguvu ya kimwili:** hutokea wakati mabavu, vitisho, au dhuluma zinatumiwa na mtu kupata kile anachokitaka.



**Nguvu ya Kisaikolojia:** pale mtu, anapoweza kutumia haiba au karama yake, na kuweza kuathiri mawazo na tabia za wengine.



# Kuna tofauti gani kati ya migogoro na vurugu?



**Mgogoro= Kutokubaliana.** Mgogoro unaweza kutatuliwa kupitia mazungumzo na vitendo vya amani.



**Vurugu= Kuwaumiza wengine kwa makusudi.** Vurugu zinaumiza sana na siku zote ni mbaya.



mgogoro huwa hauhusishi vurugu mara zote lakini kama tukishindwa **kutatua mgogoro kwa njia ya amani**, unaweza kugeuka na kuwa **vurugu.**



## Je, sikuzote mgogoro ni mbaya?

Lakini migogoro sio mibaya kila wakati ikiwa tunaitumia kujifunza na kuelewana vizuri.




Tunapozungumzia tofauti zetu kwa utulivu na kusikilizana, tunaweza kukua na kuwa marafiki bora zaidi.

# Matokeo chanya ya migogoro

## Huleta maelewano mazuri




Mgogoro unaweza kutusaidia kuelewana vizuri na kuona mambo kutoka kwenye mitazamo tofauti. Kwa njia hii, tunajifunza kuthamini maoni mbalimbali na kuimarisha kujaliana na urafiki.



## Vichocheo vya Mabadiliko

Wakati mwingine migogoro huwa ni fursa ya kubadili sheria zisizo za haki au kutafuta suluhisho litakalowanufaisha watu wote katika jamii.

## Kukua Pamoja

Mgogoro unaweza kutufundisha kushirikiana, kubadilishana mawazo, na kutatua matatizo kama timu halisi.



# Je! Tunawezaje kushughulikia migogoro kwa njia za amani na kuigeuza kuwa na matokeo chanya?

1. Zungumza kwa utulivu na utoe nafasi ya kuongea kwa pande zote.




2. Sikiliza wengine kwa makini. Hii inamaanisha kuwa hausubirii tu kuzungumza baadaye bali unatakiwa kusikiliza kwa umakini yale yanayosemwa!



3. Jaribu kufikiria jinsi ambavyo ungehisi ikiwa ungekuwa mtu yule mwingine.



4. Shirikianeni kutafuta suluhisho la haki kwa kutokubaliana kwenu. Tafuta Suluhisho Lenye Manufaa kwa Wote (Win-Win solution).



5. Pata mtazamo tofauti. Omba msaada kutoka kwa mwalimu au mtu mzima unayemwamini.




1. Katika vikundi, amueni juu ya mgogoro wa kawaida ambao hutokea shuleni miongoni mwa wanafunzi au kati ya wanafunzi na walimu.

2. Andaeni igizo linaloonyesha jinsi mgogoro unavyotokea, na **tumieni vidokezo vilivyoainishwa hapo juu kuonyesha namna ulivyotatuliwa kwa amani mwishoni.**

3. Igizeni mbele ya darasa

Marafiki zetu nchini Kenya, Tanzania, na Msumbiji wameeleza hisia zao kupitia mashairi, muziki na maigizo, na wamefanya kazi kwa pamoja katika kuwahamasisha watoto wengine kufanya shule zao ziwe salama na zenye amani zaidi!



Ninapenda ushairi, na napenda kuimba, na wewe je?

**Unataka kucheza na mimi kutumia maneno haya na kuunda mistari yako mwenyewe ya kueneza ujumbe wa amani na haki?**

Tumia maneno kwenye ukurasa unaofuatia, ongeza mengine yoyote unayopenda, na uunda kipande chako mwenyewe, kinaweza kuwa shairi au wimbo, chochote kinaruhusiwa.

Jambo la muhimu ni kwamba ujumbe wako usafiri ufike mbali sana, ukitangazwa kwa sauti kubwa katika uwanja wa shule au ukitumwa katika chupa iliyo tayari kusafiri juu ya mawimbi ya bahari!

VURUGU, UKOSEFU WA HAKI DHULMA, MAUMIVU, ELIMU, MWELE WA NURU (MWANGAZA), KIVULI, UTAJIRI, KISIWA, NJAA, MWENYE NGUVU, USIYE NA NGUVU, VITA, MVUA, KICHEKO, MIKONO, SAUTI, MTAA, BAHARI, AMANI, URAFIKI, HAKI, MOYO, TABASAMU, MKONO KWA MKONO, HESHIMA, UPATANO, UHURU, USAWA, TUMAINI, UMOJA, MSHIKAMANO, MSAADA, FURAHA.

Kijitabu hiki ni sehemu maalumu ya mradi unaoitwa **Kujenga Amani Pamoja**. Ni juhudi kubwa ya pamoja kusaidia vijana na jamii zao nchini **Kenya**, **Tanzania**, na **Msumbiji** ili kuchukua jukumu la kudumisha amani na usalama ndani ya jamii na shuleni.

Mradi huo unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya na kutekelezwa na WeWorld kwa ushirikiano na Tanzania Building Future Organization (TABUFO) na 4H nchini Tanzania, Stretchers Youth Organisation (SYO) nchini Kenya na Conselho Nacional do Voluntariado (CNV) nchini Msumbiji.

Co-funded by the European Union

**WEWORLD**

VIA SERIO 6, - 20139 MILANO - IT
T. +39 02 55231193 - F. +39 02 56816484

VIA BARACCA 3, - 40133 BOLOGNA - IT
T. +39 051 585604 - F. +39 051 582225

www.weworld.it

